# ALPHA HABARI

Toleo la Machi

31,Machi,2026


**KIKAO CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI NEEC CHAPITISHA BAJETI YA SHILINGI BILIONI 6,886,563,650 KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** UK 16

**TPSF KUSHIRIKIANA NA UBALOZI WA BRAZIL NCHINI TANZANIA KATIKA FURSA ZA KIUCHUMI.** UK 13

**JINSI MIFUMO YA UFUATILIAJI, TATHMINI NA KUJIFUNZA INAVYOBADILISHA UTIIFU WA KODI TANZANIA**

*Na Pantaleon Shoki | Mtaalamu wa Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza na Mwanzilishi, CLM Consultants Ltd* UK 05

**TRA NA URA KUSHIRIKIANA KUPAMBANA NA UKWEPAJI KODI** UK 04



# MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TATC WAHITIMISHWA KWA MAFANIKIO JIJINI ARUSHA UK 03






**BENKI YA CRDB YATENGA TZS BILIONI 2 KUWAZAWADIA WASHINDI WA SIMBANKING.**

*"Mbali na safari, kila mmoja wa washindi watano atapata TZS 1 milioni kwa ajili ya ununuzi wakati wa kukaa kwao Ulaya,"* Nshekanabo alisisitiza.

UK 09

## KODI YENYE HAKI, BIASHARA YENYE NGUVU

Na Dkt. Alphonce Dotto Massaga



*Katika mazingira ya sasa ya biashara, kodi si suala la ukusanyaji mapato pekee. Kodi ni sehemu ya uamuzi wa kuwekeza, kupanga mtaji, kupanua shughuli, kuajiri watu, na ........*

UKURASA 01



DKT. ALPHONCE DOTTO MASSAGA AKABIDHIWA CHETI CHA HESHIMA KAMA MJUMBE WA KAMATI YA USHAURI YA NM-AIST UK 07.

**UCHUMI WA KIDIGITALI NA MCHANGO WAKE KATIKA KUTEKELEZA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025-2050**

**Mwandishi: Alphonce Dotto Massaga – Alpha Associates Tanzania Limited**

UK 10

DIRA 2050




**TAWI LA ALPHA KATIKA JIJI LA MWANZA NI KITOVU CHA ELIMU KWA UMMA JUU YA MASWALA YA KODI.** UK 06

## KODI YENYE HAKI, BIASHARA YENYE NGUVU

Na Dkt. Alphonce Dotto Massaga



### UTANGULIZI WA MHARIRI

Katika toleo hili la Alpha Habari, tunawaletea wasomaji wetu makala inayogusa moja kwa moja maisha ya wafanyabiashara, wawekezaji, walipakodi na watunga maamuzi ndani ya mfumo wa kodi nchini Tanzania. Kupitia uchambuzi huu, tunaonesha namna ambavyo Tanzania Association of Tax Consultants (TATC) hutumia njia rasmi, zenye staha na uzito wa kitaaluma, kuwasilisha changamoto na mapendekezo ya maboresho ya kodi serikalini.

Ujumbe mkuu ni mmoja: mfumo bora wa kodi hujengwa kwa ushirikiano, kusikilizana, na hoja zenye mantiki.
Katika mazingira ya sasa ya biashara, kodi si suala la ukusanyaji wa mapato pekee. Kodi ni sehemu ya maamuzi ya kuwekeza, kupanga mtaji, kupanua shughuli, kuajiri watu, na kuamua kama biashara itaendelea kukua kwa utulivu au itakwama kutokana na mzigo wa taratibu. Ndiyo maana mapendekezo ya TATC yana umuhimu mkubwa kwa wakati huu. Yanagusa maisha halisi ya biashara na ubora wa usimamizi wa mapato ya Serikali.

TATC haijajenga hoja zake kwa misingi ya kupunguza wajibu wa kulipa kodi. Badala yake, imeonesha kuwa mfumo bora wa kodi ni ule unaokusanya mapato kwa haki, unaoeleweka kwa walipakodi, na unaopunguza migogoro isiyo ya lazima. Huo ndio msingi wa mazingira salama ya biashara na uthabiti wa mapato ya taifa.

**TATC inawateteaje wafanyabiashara kupitia mifumo rasmi**

Utetezi wa kweli wa wafanyabiashara hauanzi kwenye lawama, kelele au malalamiko yasiyo na mwelekeo. Unaanza kwenye uchambuzi wa sheria, uzoefu wa utekelezaji, na uwezo wa kuwasilisha mapendekezo yenye mantiki kwa lugha inayoeleweka na mamlaka husika. Hivyo ndivyo TATC inavyofanya.
Chama hukusanya changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa sheria za kodi, huzichambua kitaaluma, na kisha kuwasilisha mapendekezo serikalini kwa mfumo rasmi unaoonesha hali ilivyo sasa, tatizo lililopo, marekebisho yanayopendekezwa, na manufaa ya marekebisho hayo. Kwa njia hiyo, chama kinakuwa daraja kati ya walipakodi, wataalamu wa kodi, na Serikali.

**Maeneo makuu ambayo TATC imeonesha yanahitaji maboresho**

Kwanza, kuhusu mabadiliko ya umiliki wa kampuni, TATC imeonesha kuwa katika baadhi ya mazingira mauzo au mabadiliko ya hisa yanaweza kuzaa mzigo wa kodi unaogusa tukio lilelile zaidi ya mara moja. Hoja ya chama ni kwamba sheria itafsiriwe na kuboreshwa kwa namna inayolinda mapato ya Serikali bila kugeuza miamala halali ya biashara kuwa chanzo cha kodi inayozidi mantiki ya tukio lenyewe.

Pili, kuhusu VAT deferment kwenye mitambo na vifaa vya uwekezaji, chama kimeeleza kuwa motisha ya kuahirisha VAT haipaswi kupoteza maana yake kwa sababu ya changamoto za uwasilishaji wa taarifa. Badala ya kufanya kosa la taarifa kuwa deni kubwa la kodi, TATC inapendekeza adhabu stahiki ya kiutawala pasipo kufuta lengo la msingi la kusaidia uwekezaji.

Tatu, kuhusu utatuzi wa migogoro ya kodi, TATC imehimiza uwepo wa mfumo mpana zaidi wa ADR ili migogoro ya kodi isibaki kusubiri muda mrefu mahakamani au kwenye makubaliano yanayotegemea utayari wa upande mmoja. Kwa mfanyabiashara, suluhu ya haraka huokoa muda, fedha, na utulivu wa kufanya maamuzi.

Nne, kuhusu VAT reverse charge kwa huduma zinazoagizwa kutoka nje, chama kinaona kuwa eneo hili limebeba mzigo wa utekelezaji usioleta tija ya moja kwa moja kwa walipakodi wengi.

Tano, kuhusu salio la mikopo ya kodi iliyozidi, TATC imependekeza kuwa salio la withholding tax au provisional tax lililozidi liweze kuhamia miaka inayofuata hadi litumike kikamilifu. Hii ni hatua ya haki kwa biashara kwa sababu fedha iliyokwisha lipwa Serikalini haipaswi kubaki imefungwa kwa sababu ya ukomo wa kiutaratibu.

Sita, chama kimependekeza kuwepo kwa tahadhari za kisheria wakati taarifa binafsi, kama za benki, zinapoombwa, na pia kupunguza gharama za ukaguzi wa mahesabu kwa biashara ndogo. Haya ni maboresho yanayolinda utu wa mlipakodi na kuongeza uhalisia wa ufuataji wa sheria.

**Ujumbe wa heshima kwa uongozi wa TRA na watunga maamuzi**

Mfanyabiashara wa Tanzania anahitaji mfumo wa kodi unaompa uhakika. Anahitaji kujua kuwa juhudi zake za kuendesha biashara, kuajiri, kulipa kodi, na kukua hazitazuiwa na tafsiri zinazobadilika au taratibu zinazoongeza mzigo bila sababu ya msingi.

Kwa TRA na watunga sera, ujumbe ni kuendelea kuzipokea hoja za kitaaluma kama rasilimali ya kuboresha mifumo, si kama upinzani wa ukusanyaji wa mapato.

Kwa uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, mapendekezo ya aina hii yana thamani kubwa. Kusikiliza hoja za kitaaluma si kulegeza ukusanyaji wa mapato. Kinyume chake, ni kuimarisha uaminifu wa mfumo, kupunguza migogoro, na kujenga mazingira ambayo walipakodi wengi zaidi wanaona sababu ya kutii kwa hiari. Mfumo unaoeleweka na kukubalika hukusanya mapato kwa utulivu zaidi kuliko mfumo unaoibua hofu na sintofahamu.

Kwa mtazamo wa Alpha Habari, huu ndio ujumbe wa kisasa tunaopaswa kuusukuma: kodi iwe chombo cha maendeleo, si chanzo cha hofu; kodi iwe daraja la ushirikiano, si mzigo unaozima ari ya biashara. Wafanyabiashara wanahitaji kusikilizwa. Serikali inahitaji mapato ya uhakika. Na Tanzania inahitaji mfumo wa kodi unaoweza kubeba matarajio hayo yote kwa usawa na busara.

**Wito kwa wadau wa kodi na biashara**

Kwa wafanyabiashara, ujumbe wa msingi ni kuendelea kujenga nidhamu ya kumbukumbu sahihi, kutafuta ushauri wa kitaaluma mapema, na kushiriki kwenye majukwaa halali yanayowezesha changamoto za utekelezaji kufikishwa kwa mamlaka husika kwa sauti moja. Ushiriki huo huongeza uzito wa hoja na hujenga mazingira bora ya kufanya biashara kwa wote.

Kwa TRA na watunga sera, ujumbe ni kuendelea kuzipokea hoja za kitaaluma kama rasilimali ya kuboresha mifumo, si kama upinzani wa ukusanyaji wa mapato. Pale taasisi za umma zinaposikiliza kwa makini na kufanya maboresho yenye ushahidi, utii wa hiari huongezeka, migogoro hupungua, na heshima ya taasisi huimarika zaidi mbele ya wananchi na wawekezaji.

## Mkutano Mkuu wa Mwaka wa TATC wahitimishwa kwa mafanikio jijini Arusha

Chama cha Washauri wa Kodi Tanzania (TATC) kimeendelea kuwa jukwaa muhimu linalowakutanisha wataalamu wa kodi na uhasibu pamoja na makampuni yanayotoa huduma za ushauri wa kodi nchini Tanzania. Kupitia mchango wa chama hiki, wafanyabiashara na walipakodi wamekuwa wakipata mwongozo wa kitaaluma unaowawezesha kutekeleza wajibu wao wa kikodi kwa usahihi na kwa wakati.

Mwongozo huo pia husaidia kupunguza makosa yanayoweza kusababisha riba na adhabu za kodi, pamoja na kuboresha mawasiliano kati ya walipakodi na TRA pale panapohitajika ufafanuzi au utatuzi wa changamoto.



*Dkt. Alphonce Dotto Massaga, Mkurugenzi Mtendaji wa Alpha Associates Tanzania Limited, akipokea cheti cha udhamini wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa TATC jijini Arusha tarehe 25 Machi 2026.*

Kuanzia tarehe 25 hadi 27 Machi 2026, Chama cha Washauri wa Kodi Tanzania kilifanya Mkutano Mkuu wa Mwaka jijini Arusha. Mkutano huo uliwakutanisha wadau wa kodi, wanachama wa TATC, pamoja na maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambapo walipata nafasi ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu kodi, ikiwemo njia madhubuti za kuhamasisha matumizi ya Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Kodi za Ndani (IDRAS) kama sehemu ya kuongeza mapato ya nchi.

Akizungumza na mwandishi wa Alpha Habari jijini Arusha, Mwenyekiti wa TATC, CPA Victoria Soka, alisema kuwa mkutano huo umeendelea kuwa jukwaa muhimu la kuwaunganisha wadau wa kodi na watunga sera.

“Nimefarijika sana kuona wingi wa wanachama wa TATC katika Mkutano Mkuu wa mwaka huu. Hii ni hatua nzuri katika kuhakikisha tunasonga mbele kama jumuiya kwa umoja wetu,” alisema CPA Victoria Soka.

Kwa upande wake, Dkt. Alphonce Dotto Massaga, Mkurugenzi Mtendaji wa Alpha Associates Tanzania Limited, alisema jukwaa hilo la pamoja litaimarisha huduma za ushauri wa kikodi kupitia mafunzo yaliyopatikana katika mkutano huo.

“Tumejifunza mambo mengi, lakini kwa ujumla mkutano huu wa mwaka utaenda kubadilisha mfumo wa utoaji elimu ya kodi kwa umma na kwa wateja wetu tunaowahudumia,” alisema Dkt. Alphonce Dotto Massaga.

Mkutano Mkuu wa Mwaka wa TATC umefanyika kwa siku tatu, huku Alpha Associates Tanzania Limited ikiwa miongoni mwa wadhamini wa mkutano huo kwa mwaka 2026. Kampuni hii imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuhudumia jamii kupitia elimu ya kodi na usimamizi wa biashara kwa zaidi ya miaka 25.



*Wajumbe na wanachama wa TATC wakifuatilia majadiliano wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika jijini Arusha.*

# TRA NA URA KUSHIRIKIANA KUPAMBANA NA UKWEPAJI KODI

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Mapato ya Uganda (URA) wamekubaliana kuimarisha ushirikiano katika kupambana na ukwepaji kodi, hususan kwa kudhibiti vitendo vya magendo vinavyotokea kati ya nchi hizo mbili.

Akizungumza wakati wa ziara ya maofisa wa URA nchini Tanzania, iliyoongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa URA, Emmanuel Katonge, katika kikao kilichofanyika kwenye ofisi za TRA jijini Dar es Salaam tarehe 25 Machi 2026, Kamishna Mkuu wa TRA, CPA Yusuph Juma Mwenda, alisema kuwa ushirikiano huo utawezesha nchi hizo mbili kudhibiti ipasavyo vitendo vya magendo na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.
Alisema TRA imeendelea kuwa na uhusiano mzuri wa muda mrefu na URA katika utendaji kazi, ikiwa ni pamoja na kubadilishana taarifa na uzoefu wa kiutendaji.
Aidha, aliwaonya wafanyabiashara wasio waaminifu wanaoingiza mchele nchini Uganda huku wakidai kuwa unatoka Tanzania, akibainisha kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika kufanya udanganyifu huo.

Kamishna Mkuu huyo aliongeza kuwa TRA itaendelea kuwezesha biashara kati ya nchi hizo mbili, ikiwemo kuimarisha ushirikiano wa kiforodha na kikodi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya URA, Emmanuel Katonge, alisema kuwa URA itaendelea kushirikiana kwa karibu na TRA katika masuala ya kodi pamoja na kuzuia uingizaji wa bidhaa zilizopigwa marufuku katika nchi zote mbili.
Naye Kamishna Mkuu wa URA, John Musinguzi Rujoki, alisema kuwa TRA na URA wamekuwa wakishirikiana katika mikakati mbalimbali inayolenga kupanua wigo wa kodi na kuongeza mchango wa mapato ya kodi kwa maendeleo ya taifa. Aliongeza kuwa taasisi hizo mbili zinaendelea kunufaika kupitia kubadilishana utaalamu, maarifa na rasilimali watu.




*Viongozi wa TRA na URA wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kikao cha ushirikiano kilichofanyika jijini Dar es Salaam.*

ALPHA HABARI
Toleo la Machi
31,Machi,2026

# JINSI MIFUMO YA UFUATILIAJI, TATHMINI NA KUJIFUNZA INAVYOBADILISHA UTIIFU WA KODI TANZANIA

*Na Pantaleon Shoki*

Safari ya Tanzania kuelekea Dira 2050 inategemea nguzo muhimu ambayo mara nyingi hupuuzwa: uhamasishaji wa rasilimali za ndani. Bila mapato thabiti ya kodi, huduma za jamii hukwama, miundombinu hubaki nyuma, na mafanikio ya maendeleo hupungua. Hata hivyo, utiifu peke yake hautoshi. Tanzania inahitaji utamaduni wa utiifu unaozingatia ushahidi, ambapo ufuatiliaji, tathmini na kujifunza vinakuwa injini ya kuendesha utendaji wa kodi kwa muda mrefu.

Huu ndio mwelekeo wa mabadiliko ambao Alpha Associates Tanzania Limited inaleta katika huduma zake za kitaaluma. Ikiwa na shughuli Dar es Salaam, Mwanza na Arusha, Alpha Associates inatoa huduma za uhasibu, utiifu wa kodi na ushauri wa biashara, ikiwezesha watu binafsi, biashara ndogo na za kati, pamoja na makampuni yanayokua, kudumisha kumbukumbu zinazokidhi sheria, kutekeleza wajibu wa TRA, na kufanya maamuzi kwa kutumia taarifa sahihi za kifedha.

Lakini utiifu ni hatua ya kwanza tu. Mabadiliko ya kweli yanahitaji kupima matokeo, si kazi zilizotekelezwa pekee.

Kupitia tathmini za uwezo zilizopangwa, dashibodi za ufuatiliaji wa matokeo, na mafunzo ya wafanyakazi yanayolingana na mahitaji ya TRA, mifumo ya ufuatiliaji, tathmini na kujifunza inawezesha makampuni kama Alpha Associates kwenda zaidi ya utiifu wa kawaida na kufikia utiifu makini, ambapo takwimu huongoza maamuzi, ushahidi huunda mkakati, na kila shilingi inayokusanywa huchangia Dira 2050.

Biashara inapowasilisha kwa wakati taarifa za VAT, PAYE, SDL au WHT, hiyo ni hatua muhimu. Lakini iwapo taarifa hizo zinaakisi kumbukumbu sahihi, hazisababishi hatari ya faini, na zinachangia ukuaji endelevu wa biashara, hapo ndipo tunapata matokeo ya kweli. Mifumo ya ufuatiliaji, tathmini na kujifunza husaidia kutofautisha kati ya utekelezaji wa kawaida na matokeo yenye tija.

Chini ya uongozi wa Dkt. Alphonce Dotto Massaga, Alpha Associates inasisitiza umuhimu wa kumbukumbu sahihi, udhibiti wa hatari, na mwongozo unaosaidia wateja kufanya maamuzi yenye ujasiri huku wakidumisha heshima mbele ya TRA. Hapo ndipo mifumo ya ufuatiliaji wa ndani huongeza thamani kwa kufuatilia utendaji wa utiifu kwa wakati, kutambua mapungufu yanayojirudia, na kuzalisha maarifa yanayopunguza uwezekano wa ukaguzi usio wa lazima.


**Kuhusu mwandishi**

*Pantaleon Shoki ni Mwanzilishi na Mkurugenzi wa CLM Consultants Ltd, na Katibu Mtendaji wa Chama cha Wataalamu wa Tathmini Tanzania (TanEA). Kwa sasa anasaidia uimarishaji wa uwezo wa MEL katika Alpha Associates Tanzania Limited.*



*"Utiifu si lengo la mwisho. Ni safari inayopimwa kila wakati."*

ALPHA HABARI
Toleo la Machi
31,Machi,2026



# Tawi la Alpha katika jiji la Mwanza ni kitovu cha elimu kwa umma juu ya maswala ya kodi.



Alpha Associates Tanzania Limited, kupitia tawi lake la Mwanza lililopo katika jengo la Nyanza Cooperative Union, Ghorofa ya Tatu, limeendelea kuwa kitovu cha utoaji wa elimu kwa umma juu ya masuala ya kodi na biashara katika Kanda ya Ziwa.

Mfumo wa EFD (Electronic Fiscal Device) ni mfumo wa kielektroniki uliowekwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kurekodi mauzo ya biashara na kutoa risiti za kodi zinazothibitishwa na kutumwa moja kwa moja kwenye mfumo mkuu wa TRA. Mfumo huu ulianza kutumika rasmi nchini Tanzania mwaka 2010 kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa kodi, kupunguza ukwepaji wa kodi, na kuweka kumbukumbu sahihi za mauzo ya biashara.

Katika hatua za awali, matumizi ya mashine za EFD yalikuwa ya lazima kwa wafanyabiashara waliosajiliwa VAT, lakini baadaye matumizi yake yakaendelea kupanuliwa kwa wafanyabiashara wengine kadri mfumo wa usimamizi wa kodi ulivyoendelea kuimarishwa.

Mnamo tarehe 9 Machi 2026, Meneja wa Tawi la Mwanza wa Alpha Associates Tanzania Limited, Lucas Mabula, alipokea ugeni kutoka kampuni ya Kenlight Enterprises, uliolenga kupata mafunzo maalum ya namna bora ya kutumia mashine za EFD.


Akizungumza na Alpha Habari, Lucas Mabula alisema kuwa huduma zinazotolewa na Alpha Associates upande wa Mwanza ni sehemu muhimu ya kutatua changamoto za biashara na kodi katika jamii ya Kanda ya Ziwa.

“Alpha Associates imeendelea kuwa mshirika muhimu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kupitia huduma mbalimbali tunazotoa, hususan elimu ya mlipakodi na ushauri wa kikodi,” alisema Lucas Mabula.

Kwa upande wake, Fred Mengi kutoka Kenlight Enterprises alieleza kufurahishwa na elimu aliyoipata, akisema kuwa mafunzo hayo yatasaidia kuboresha utendaji wa biashara yake.

“Nimefurahishwa na huduma niliyoipata hapa Alpha Mwanza. Elimu hii itanisaidia kuboresha utendaji wangu wa biashara,” alisema Fred Mengi.

Tawi la Mwanza limeendelea kuwahudumia wafanyabiashara na wadau mbalimbali katika Kanda ya Ziwa, huku huduma bora zikiendelea kuwa msingi wa utekelezaji wa majukumu ya watumishi wa Alpha Associates Tanzania Limited.



*Meneja wa Tawi la Mwanza, Lucas Mabula, akiwa katika mafunzo ya matumizi ya mashine za EFD na mgeni kutoka Kenlight Enterprises.*



# Dkt. Alphonce Dotto Massaga akabidhiwa cheti cha heshima kama mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya NM-AIST.

Chuo cha Nelson Mandela African Institution of Science and Technology (NM-AIST) kilichopo Arusha ni moja ya taasisi muhimu barani Afrika inayojikita katika sayansi, teknolojia na ubunifu. Chuo hiki kina mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya teknolojia nchini Tanzania kupitia mikakati endelevu inayolenga maendeleo ya muda mrefu.

NM-AIST inaweka mkazo katika tafiti zinazogusa changamoto za ndani kama kilimo, afya, nishati na maji. Kupitia tafiti hizo, wanafunzi na watafiti huendeleza suluhisho za kiteknolojia zinazoweza kutumika moja kwa moja katika jamii.

Katika kufanikisha azma hiyo, Kamati ya Ushauri ya chuo hicho ina nafasi muhimu katika kusaidia maendeleo ya mitaala, utoaji wa ushauri wa kitaaluma, na ustawi wa taasisi kwa ujumla.

Mnamo tarehe 25 Machi 2026, wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya NM-AIST walikutana jijini Arusha kujadili mikakati mbalimbali ya kuimarisha maendeleo ya chuo hicho. Katika kikao hicho, wadau walieleza namna ambavyo mikakati endelevu inaweza kuongeza tija katika taasisi hiyo ya elimu.

Kwa upande wake, Dkt. Alphonce Dotto Massaga, Mkurugenzi Mtendaji wa Alpha Associates Tanzania Limited na mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya NM-AIST, alisema kuwa lengo kuu ni kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora sambamba na kukuza mchango wa teknolojia katika maendeleo ya taifa.

“Kamati ya Ushauri ni nguzo muhimu katika kusukuma mbele maendeleo ya chuo sambamba na sekta nzima ya teknolojia nchini,” alisema Dkt. Alphonce Dotto Massaga.

Kikao hicho kilihitimishwa kwa maazimio mbalimbali yaliyolenga kuongeza ufanisi wa kiutendaji, kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa, na kuendeleza maono chanya ya kukifanya chuo hicho kuwa kitovu imara cha sayansi, teknolojia na ubunifu.

Majukumu makubwa ya kamati ya ushauri NM-IAST ni kuunganisha tafiti na bunifu zinazofanywa na wanafunzi wa chuo cha Nelson Mandela na kuzileta katika soko la biashara na uwekezaji katika sekta ya teknolojia Nchini



*Dkt. Alphonce Dotto Massaga akikabidhiwa cheti cha heshima kama mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya NM-AIST.*



*Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya NM-AIST katika kikao maalum kilichofanyika jijini Arusha tarehe 25 Machi 2026.*

KONA YA DAR ES SALAAM

## IFAHAMU KODI YA FORODHA NA TIJA YAKE KATIKA KUCHECHEMUA UCHUMI WA TANZANIA

*Imeandaliwa na:(Azaria Suleiman Mhasibu |Meneja wa tawi-Dar es salaam, Alpha Associates Tanzania Limited)*



**+255 716 486 028**

Kodi ya forodha nchini Tanzania ni aina ya kodi inayotozwa kwa bidhaa zinazoingizwa (imports) au zinazotoka nje ya nchi (exports). Mfumo huu unasimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) chini ya sheria za forodha na mikataba ya kikanda kama ule wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kimsingi, kodi ya forodha inafanya kazi kwa hatua kadhaa. Kwanza, mfanyabiashara au mwagizaji anapaswa kutangaza bidhaa zake kwa kujaza nyaraka maalum za forodha (customs declaration). Nyaraka hizi huonesha aina ya bidhaa, thamani yake, nchi ilikotoka, na matumizi yake. Baada ya hapo, mamlaka ya forodha hufanya tathmini ya thamani ya bidhaa (customs valuation) ili kubaini kiwango cha kodi kinachostahili kulipwa. Kodi hii inaweza kujumuisha ushuru wa forodha (import duty), VAT ya bidhaa zinazoingizwa, na tozo nyingine kama excise duty kulingana na aina ya bidhaa.

Aidha, bidhaa hukaguliwa ili kuhakikisha zinazingatia viwango vya ubora na usalama kabla ya kuruhusiwa kuingia sokoni. Mfumo wa kidigitali kama TANCIS (Tanzania Customs Integrated System) hutumika kurahisisha taratibu hizi, kupunguza ucheleweshaji na kuongeza uwazi. Baada ya mlipaji kukamilisha malipo ya kodi husika, ndipo bidhaa huruhusiwa kutoka bandarini au mipakani.

Kodi ya forodha ina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi. Kwanza, ni chanzo muhimu cha mapato ya serikali. Mapato haya hutumika kugharamia huduma za kijamii kama elimu, afya, miundombinu, na usalama.

Pili, kodi hii hulinda viwanda vya ndani kwa kupunguza ushindani usio wa haki kutoka kwa bidhaa za nje. Kwa mfano, bidhaa zinazoingizwa zinaweza kutozwa ushuru mkubwa ili kuwapa wazalishaji wa ndani nafasi ya kukua na kushindana.

Tatu, kodi ya forodha huchochea maendeleo ya viwanda na uzalishaji wa ndani kwa kuweka mazingira yanayohamasisha uwekezaji wa ndani.

Nne, inasaidia kudhibiti uingizaji wa bidhaa hatarishi au zisizokidhi viwango, hivyo kulinda afya na usalama wa wananchi. Pia, mfumo wa forodha husaidia katika ukusanyaji wa takwimu muhimu za biashara ya kimataifa ambazo hutumika kupanga sera za kiuchumi.

Hata hivyo, kodi ya forodha inaweza kuwa na changamoto kama vile ucheleweshaji wa mizigo, gharama kubwa kwa wafanyabiashara, na uwezekano wa ukwepaji kodi. Hivyo, maboresho ya mifumo ya kidigitali na usimamizi madhubuti ni muhimu ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha kuwa kodi ya forodha inaendelea kuchangia ipasavyo katika kukuza uchumi wa Tanzania.



## BENKI YA CRDB YATENGA TZS BILIONI 2 KUWAZAWADIA WASHINDI WA SIMBANKING.

Katika jitihada zake za kuendelea kukuza ushirikishwaji wa fedha za kidijitali miongoni mwa Watanzania mnamo Machi 25, 2026 , Benki ya CRDB imetenga TZS 2 bilioni zitakazotolewa kwa wateja watakaoibuka kuwa watumiaji bora wa huduma zake za SimBanking. Mfuko huo ulitangazwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Frederick Nshekanabo, wakati wa uzinduzi wa msimu wa sita wa kampeni ya “Benki ni SimBanking”, ambayo imeimarishwa mwaka huu chini ya kaulimbiu ya “SiMBanking Benki Kimpango Wako” “Tutakuwa na washindi kila wiki, kila mwezi, na kila robo mwaka kabla ya kutangaza zawadi kubwa Nshekanabo.




Tofauti na misimu iliyopita ambapo mshindi mmoja wa jumla angepokea gari, kampeni ya mwaka huu inaleta zawadi za kiubunifu zaidi. Badala ya mshindi mmoja wa tuzo kuu, washindi watano kila mmoja atapata safari ya siku saba kwenda Ulaya, kutembelea nchi tatu zitakazotangazwa baadaye. "Mbali na safari, kila mmoja wa washindi watano atapata TZS 1 milioni kwa ajili ya ununuzi wakati wa kukaa kwao Ulaya," Nshekanabo alisisitiza.

Mbali na washindi hao wa safari za Ulaya, washindi wengine watano watatunukiwa ziara ya siku tatu iliyodhaminiwa kikamilifu na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika droo za robo mwaka

Zawadi nyingine za robo mwaka zitakwenda kwa wateja wanaofanya miamala kupitia mawakala wa Benki ya CRDB au wanaotumia huduma zisizo na kadi, ambao watajishindia televisheni za inchi 65. Jumla ya washindi 33 (11 kwa kila robo) watapata zawadi hizi. Wateja wanaotumia huduma za kuweka tokeni au kutuma pesa kupitia SimBanking kwa wateja wasio wa CRDB pia

Kwa wateja wanaotumia mawakala wa Benki ya CRDB, Nshekanabo alisema: “Tutatoa fedha taslimu jumla ya TZS milioni 60 kwa washindi watatu. Mshindi wa kwanza atapata TZS milioni 30, wa pili TZS milioni 20 na wa tatu TZS milioni 10.” Kila wiki na kila mwezi, kampeni pia itatoa zawadi za pesa taslimu, simu mahiri na kompyuta mpakato kwa wateja, mawakala na wanafunzi wa vyuo vikuu kote nchini. Akizungumzia kustahiki, Nshekanabo alibainisha kuwa kila Mtanzania ana nafasi ya kushinda kwa kutumia SimBanking. "Hata ukifungua akaunti leo na kuanza kutumia SimBanking, utaingizwa kwenye droo zetu," alisema.

Benki ya CRDB imekuwa ikiendesha kampeni hii kwa miaka kadhaa ili kuhamasisha wateja na wananchi kwa ujumla kutumia huduma za kibenki kidijitali, sambamba na mabadiliko ya kimataifa ya kuachana na miamala ya fedha taslimu. Athari za kampeni hii zinaendelea kukua, ambapo zaidi ya 95% ya miamala yote ndani ya Benki ya CRDB sasa inafanywa kupitia mifumo mbalimbali ya kidijitali. "Kupitia SimBanking, mojawapo ya majukwaa yetu muhimu ya kidijitali, tumepata mabadiliko makubwa katika utoaji wa huduma. Wateja sasa wanaweza kufungua akaunti, kufanya miamala, kulipa bili, kupata mikopo, kufanya uwekezaji, kununua bima, na kusimamia fedha zao kikamilifu kupitia simu zao za mkononi bila kutembelea tawi la benki," Nshekanabo alimalizia kwa kusema hivyo.

ALPHA HABARI
Toleo la Machi
31,Machi,2026

# UCHUMI WA KIDIGITALI NA MCHANGO WAKE KATIKA KUTEKELEZA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025-2050

Mwandishi: Alphonce Dotto Massaga – Alpha Associates Tanzania Limited

**Utangulizi**

Uchumi wa kidijitali una mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025–2050 kwa kuharakisha ukuaji wa uchumi, kuongeza ufanisi, na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Mchango huo unaonekana katika maeneo mbalimbali muhimu ya maendeleo ya taifa.

Kwanza, uchumi wa kidijitali unafungua fursa mpya za ajira kupitia biashara mtandaoni, ubunifu wa teknolojia, kazi za mtandao, na huduma za mbali. Hali hii huongeza kipato cha wananchi na kusaidia kupunguza ukosefu wa ajira, hasa kwa vijana.

Pili, matumizi ya mifumo ya kidijitali kama EFD, malipo ya kielektroniki, na mifumo ya kodi yanaongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kupunguza ukwepaji wa kodi, na kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Tatu, teknolojia inarahisisha utoaji wa huduma za umma kupitia mifumo ya e-government, ikijumuisha huduma za afya, elimu ya mtandaoni, usajili na utoaji wa leseni kwa njia ya kidijitali. Hii hupunguza urasimu na kuongeza upatikanaji wa huduma kwa haraka na kwa gharama nafuu.

Nne, uchumi wa kidijitali unasaidia kukuza sekta binafsi na ubunifu kwa kuwapa wajasiriamali fursa ya kufikia masoko mapana zaidi, kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara, na kuongeza ushindani wa bidhaa na huduma.

Tano, uchumi wa kidijitali unaimarisha ujumuishi wa kifedha kupitia huduma kama M-Pesa, Tigo Pesa, Airtel Money na majukwaa mengine ya kifedha. Kupitia huduma hizi, wananchi wengi zaidi, hasa wa maeneo ya vijijini, wameweza kupata huduma za kifedha kwa urahisi, jambo linalosaidia kupunguza umaskini na kuongeza ushiriki katika uchumi rasmi.

Sita, mifumo ya kidijitali inasaidia kuongeza uwazi na kupambana na rushwa kwa sababu inarekodi miamala, inapunguza mwingiliano wa ana kwa ana, na kuongeza uwajibikaji katika utoaji wa huduma na usimamizi wa mapato.

Saba, teknolojia ya kidijitali inaimarisha sekta za uzalishaji kama kilimo, viwanda na huduma. Kupitia kilimo cha kisasa, usimamizi wa viwanda kwa njia ya kiotomatiki, na matumizi ya majukwaa ya kidijitali katika huduma, taifa hupata ongezeko la tija na uzalishaji, jambo ambalo ni msingi wa uchumi imara.

Kwa ujumla, uchumi wa kidijitali ni kichocheo muhimu katika kufanikisha Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025–2050 kwa sababu unaharakisha maendeleo, unapanua fursa za kiuchumi, na unaongeza ufanisi katika sekta mbalimbali. Ili kunufaika zaidi, ni muhimu kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya TEHAMA, elimu ya kidijitali, na sera rafiki kwa maendeleo ya teknolojia.

DIRA 2050

ALPHA HABARI
Toleo la Machi
31,Machi,2026

KONA YA ARUSHA

# MAJUKWAA YA KIMATAIFA YA KIDIGITALI NA UCHUMI ENDELEVU WA TANZANIA

*imeandaliwa na:(Naomi Ephraim Mhasibu |Meneja wa tawi- Arusha Alpha associates Tanzania limited)*



+255 712 123 579

Majukwaa ya kimataifa ya kidijitali kama Netflix hulipa kodi nchini Tanzania kupitia mfumo wa kodi ya huduma za kidijitali (Digital Services Tax - DST) pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa huduma zinazotolewa kwa watumiaji waliopo nchini. Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeweka utaratibu maalum unaowalazimisha watoa huduma wa nje (non-resident service providers) kujisajili na kulipa kodi hata kama hawana ofisi ya moja kwa moja nchini.

Kwanza, kwa upande wa VAT, majukwaa kama Netflix hutoza kodi ya asilimia 18 kwa watumiaji wa Tanzania wanaolipia huduma zao mtandaoni. Hii ina maana kuwa mteja anapolipia usajili wa kila mwezi, sehemu ya malipo hayo hujumuisha VAT ambayo kampuni husika hukusanya na kuwasilisha TRA. Kwa mfano, kama gharama ya usajili ni dola 10, basi kiasi hicho kinaweza kujumuisha VAT ambayo inalipwa kwa serikali ya Tanzania.

Pili, kuna kodi ya huduma za kidijitali (DST) ambayo hulenga mapato yanayotokana na huduma za kidijitali zinazotolewa nchini.

Kwa kawaida, DST hukokotolewa kama asilimia fulani ya mapato ghafi yanayotokana na watumiaji wa ndani ya Tanzania. Hii ina maana kuwa Netflix hulipa kodi kulingana na idadi ya watumiaji wake nchini na kiasi wanacholipa.

Mfano mwingine ni Google na Meta Platforms (mmiliki wa Facebook na Instagram). Kampuni hizi hulipa kodi kupitia matangazo ya kidijitali. Mfanyabiashara wa Tanzania anapolipia tangazo Facebook au Google Ads, gharama hiyo hujumuisha VAT na pia huchangia mapato yanayotozwa DST.
Aidha, TRA imeanzisha mfumo wa usajili wa mtandaoni kwa kampuni za nje ili kuhakikisha zinatii sheria za kodi bila kuwa na uwepo wa kimwili nchini. Hii imeongeza uwazi na ukusanyaji wa mapato ya serikali kutoka sekta ya kidijitali inayokua kwa kasi.

Kwa ujumla, mfumo huu unasaidia Tanzania kupata mapato kutoka kwa biashara za kimataifa zinazofanya kazi mtandaoni bila uwepo wa moja kwa moja. Pia unaleta ushindani sawa kati ya kampuni za ndani na za nje.

Hata hivyo, changamoto bado zipo kama ugumu wa kufuatilia mapato halisi na utekelezaji kwa kampuni zisizo na ushirikiano wa karibu.

MAJUKWAA YA KIMATAIFA YA KIDIGITALI

TANZANIA PRIVATE SECTOR FEDERATION

## TPSF KUSHIRIKIANA NA UBALOZI WA BRAZIL NCHINI TANZANIA KATIKA FURSA ZA KIUCHUMI.

Katika jitihada za kuimarisha uhusiano wa kimataifa na ushirikiano wa kiuchumi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Bw. Raphael Maganga, alikutana na Mheshimiwa Gustavo Martins Nogueira, Balozi wa Brazil nchini Tanzania, tarehe 27 Machi 2026.

Majadiliano hayo yalilenga kutafuta njia za kuimarisha biashara, uwekezaji na ukuaji wa uchumi kati ya Tanzania na Brazil. Wadau hao walisisitiza umuhimu wa kuoanisha fursa za pande zote mbili kwa lengo la kufungua nafasi mpya za ushirikiano katika sekta muhimu za uchumi.

Ziara hiyo ya heshima ililenga kufufua ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Brazil, kupanua biashara baina ya nchi hizo mbili, kushughulikia changamoto za usawa wa biashara, na kuimarisha ushirikiano wa sekta binafsi katika kilimo, nishati, madini na teknolojia.

Aidha, mazungumzo yaligusa pia umuhimu wa kubadilishana maarifa na kuendeleza ubia utakaoisaidia Tanzania kunufaika na uzoefu wa Brazil, hasa katika maeneo ya usindikaji wa mazao ya kilimo na uendelezaji wa masoko yanayoibukia.



Balozi Nogueira alisisitiza dhamira ya Brazil ya kuimarisha uhusiano huo, akisema kuwa Brazil inaona uwezekano mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kwamba kwa kuoanisha uwezo wa pande zote mbili, mataifa hayo yanaweza kupata matokeo yenye manufaa ya pamoja.

Kwa upande wake, Bw. Maganga alisema kuwa mazungumzo hayo yanaashiria hatua muhimu kuelekea biashara yenye usawa zaidi. Aliongeza kuwa kwa kukuza uhusiano kati ya wafanyabiashara wadogo na wa kati pamoja na kuvutia wawekezaji kutoka Brazil, Tanzania inaweza kuongeza ajira, uhamishaji wa maarifa, na maendeleo ya teknolojia.

Kwa ujumla, mkutano huo unaonesha mwanzo mzuri wa kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Brazil kwa manufaa ya sekta binafsi na uchumi wa nchi zote mbili.




*Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Bw. Raphael Maganga, akiwa na Balozi wa Brazil nchini Tanzania, Mheshimiwa Gustavo Martins Nogueira, baada ya mazungumzo ya ushirikiano wa kiuchumi.*

ALPHA HABARI

Toleo la Machi

31,Machi,2026

KONA YA MWANZA

## FAHAMU UTOFAUTI KATI YA WALIPA KODI WADOGO NA WAKUBWA

*Imeandaliwa na: (Lucas MabulaMhasibu|Meneja wa tawi - Mwanza-Alpha Associates Tanzania Limited)*



+255 712 123 579

Tofauti kati ya walipa kodi wadogo na walipa kodi wakubwa nchini Tanzania inaeleweka zaidi kwa kuangalia vigezo vya mapato, ukubwa wa biashara, aina ya kodi wanazolipa pamoja na namna wanavyosimamiwa na mamlaka ya kodi kama Tanzania Revenue Authority.

Kwanza, walipa kodi wadogo ni wale wenye biashara ndogo ndogo au kipato cha chini. Mara nyingi hawa ni wafanyabiashara wa rejareja, wajasiriamali wa mitaani, au watoa huduma binafsi kama mafundi na mama lishe. Kwa kawaida, mapato yao hayazidi kiwango kilichowekwa na serikali kwa ajili ya kuingia kwenye mfumo wa kodi ya mapato ya kawaida. Badala yake, hulipa kodi kwa mfumo rahisi zaidi kama vile kodi ya makadirio (presumptive tax). Mfumo huu huwekwa ili kupunguza ugumu wa ulipaji kodi na kuwahamasisha watu wengi kuingia kwenye mfumo rasmi wa uchumi. Aidha, walipa kodi wadogo hawalazimiki kutumia mifumo tata ya kihasibu, na mara nyingi hawatumii mashine za kielektroniki za EFD kwa kiwango kikubwa.

Kwa upande mwingine, walipa kodi wakubwa ni makampuni makubwa, viwanda, taasisi na biashara zenye mtaji mkubwa na mapato makubwa. Hawa hujumuisha pia kampuni za kimataifa zinazofanya shughuli zao nchini Tanzania. Walipa kodi wakubwa hulipa kodi mbalimbali kama kodi ya mapato ya kampuni, kodi ya ongezeko la thamani (VAT), ushuru wa forodha, na kodi za mishahara (PAYE). Tofauti na walipa kodi wadogo, hawa wanatakiwa kuwa na mifumo imara ya uhasibu, kufanya ukaguzi wa hesabu mara kwa mara, na kuwasilisha taarifa sahihi za kifedha kwa TRA. Pia hutumia kikamilifu mashine za EFD na mifumo ya kidigitali katika kuripoti mapato yao.

Tofauti nyingine muhimu ni namna wanavyosimamiwa. Walipa kodi wakubwa husimamiwa kwa karibu zaidi na TRA kupitia idara maalum inayojihusisha na walipa kodi wakubwa (Large Taxpayers Department). Ukaguzi wa mara kwa mara hufanyika ili kuhakikisha wanazingatia sheria za kodi. Walipa kodi wadogo, kwa upande wao, husimamiwa kwa njia rahisi zaidi, na mara nyingi hupewa elimu ya kodi ili kuwasaidia kuelewa wajibu wao.

Kwa ujumla, walipa kodi wakubwa huchangia sehemu kubwa ya mapato ya serikali kutokana na ukubwa wa biashara zao, wakati walipa kodi wadogo huchangia kwa wingi wao na kusaidia kupanua wigo wa kodi nchini. Hivyo, makundi yote mawili ni muhimu katika kukuza uchumi wa Tanzania na kuhakikisha serikali inapata mapato ya kutosha kwa ajili ya maendeleo ya taifa.



Biashara ndogondogo



Biashara Kubwa

ALPHA HABARI
Toleo la Machi
31,Machi,2026

# ZIFAHAMU SIFA ZA KODI YA KIDIGITALI (DIGITAL TAXATION)

Kodi ya kidigitali hutegemea mifumo ya kielektroniki kama vile mashine za EFD, mifumo ya mtandao, na majukwaa ya malipo ya kidigitali. Taasisi kama Tanzania Revenue Authority hutumia mifumo hii kukusanya taarifa kwa wakati halisi, Mfumo huu huruhusu mamlaka za kodi kufuatilia miamala ya biashara papo hapo, hivyo kupunguza mianya ya ukwepaji kodi.

Kodi ya kidigitali huongeza uwazi kwa sababu taarifa zote za miamala huhifadhiwa kwenye mfumo, hivyo kurahisisha ukaguzi na kupunguza udanganyifu, Kwa kutumia teknolojia, gharama za ukusanyaji kodi hupungua kwa sababu taratibu nyingi zinafanyika kiotomatiki bila kutumia nguvu kazi kubwa.

Mifumo ya kidigitali huhifadhi taarifa kwa muda mrefu bila kupotea kirahisi, tofauti na kumbukumbu za karatasi, Walipakodi wanaweza kulipa kodi, kuwasilisha marejesho (returns), na kupata taarifa kupitia mifumo ya mtandaoni bila kufika ofisini.










Kwa kuwa taarifa zinarekodiwa moja kwa moja, ni vigumu kwa wafanyabiashara kuficha mapato yao, hivyo kuongeza mapato ya serikali ,Mifumo ya kodi ya kidigitali huunganishwa na mifumo mingine kama benki, mitandao ya simu, na taasisi za kifedha kwa urahisi.

Teknolojia hutumika kulinda taarifa za walipakodi kwa kutumia mifumo ya usalama kama encryption na authentication, Ili kufaidika na mfumo huu, walipakodi wanahitaji kuwa na uelewa wa msingi wa matumizi ya teknolojia.

Mfumo wa kidigitali hupunguza ukwepaji kodi, hivyo kusaidia taasisi kama Tanzania Revenue Authority kukusanya mapato kwa ufanisi zaidi, Walipakodi wanaweza kulipa kodi kupitia simu, benki, au mtandao bila kufika ofisini, Kwa kuwa mifumo ni ya kiotomatiki, inapunguza mwingiliano wa moja kwa moja kati ya mlipakodi na afisa wa kodi.









## KIKAO CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI NEEC CHAPITISHA BAJETI YA SHILINGI BILIONI 6,886,563,650 KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Kikao cha Baraza la Wafanyakazi kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kimepitisha bajeti ya kiasi cha Shilingi Bilioni6,886,563,650 kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Haya yamefanyika katika Ukumbi wa Lush Garden uliopo Arusha. Kikao hicho kimeongozwa na Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza Ndg. Gwakisa Bapala, Katibu wa TUGHE Mkoa wa Dodoma Ndg. Samwel Nyungwa, mwakilishi wa TUGHE Taifa Ndg. Tamsoni Mshighati wajumbe wa Baraza.

Akifungua kikao hicho Kaimu Katibu Mtendaji alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ongezeko la bajeti kwenye Taasisi kuanzia Julai 2025.

*"Nichukue nafasi hii kwa kuwapongeza kwa kufika kwenye kikao hiki na wafanyakazi wote wawe huru kutoa maoni na sisi kama menejimenti tutayachukua yale yote ya msingi na kuyafanyia kazi"* aliongeza Kaimu Katibu Mtendaji.
Naye Katibu wa TUGHE Mkoa, alilipongeza Baraza kwa kikao kizuri na kuahidi kuendelea kutoa Ushirikiano kwa Baraza pale utakapohitajika.

Bajeti hio inatazamiwa kuleta athari chanya katika kuongeza vipato vya wajasiriamali sambamba na ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa ujumla kupitia uwezeshaji kiuchumi unatazamiwa kufanywa na NEEC



KONA YA SHERIA

# IFAHAMU SHERIA ZA KODI YA FORODHA TANZANIA

*Imeandaliwa na: (Deogratias A. Massaga Mwanasheria Alpha Associates Tanzania Limited)*



+255 764 017 324

Kodi ya forodha ni moja ya vyanzo vikuu vya mapato ya serikali nchini Tanzania, na inasimamiwa na Mamlaka ya Mapato (TRA). Sheria hizi zimewekwa ili kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa bidhaa nje na ndani ya nchi, kuhakikisha usawa wa biashara, na kulinda uchumi wa taifa.

Kimsingi, sheria za kodi ya forodha zinatokana na mfumo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia, East African Community (EAC), ambapo nchi wanachama hutumia sheria zinazofanana ili kurahisisha biashara za kikanda. Sheria kuu inayotumika ni East African Community Customs Management Act (EACCMA), ambayo inaelekeza namna ya kukokotoa kodi, taratibu za forodha, pamoja na adhabu kwa wanaokiuka sheria.

Moja ya vipengele muhimu vya sheria hizi ni uainishaji wa bidhaa (tariff classification). Kila bidhaa ina nambari maalum (HS Code) ambayo hutumika kubaini kiwango cha ushuru kinachopaswa kulipwa. Aidha, thamani ya bidhaa (customs valuation) huamuliwa kwa kuzingatia bei halisi ya ununuzi pamoja na gharama za usafirishaji na bima.

Sheria pia zinahitaji waagizaji na wasafirishaji wa bidhaa kujisajili na TRA na kupata namba ya mlipakodi (TIN). Bila kufuata utaratibu huu, mfanyabiashara hataruhusiwa kuingiza au kusafirisha bidhaa kisheria. Vilevile, tamko la forodha (customs declaration) linapaswa kujazwa kwa usahihi ili kuepuka adhabu au ucheleweshaji wa mizigo bandarini.

Katika kulinda maslahi ya taifa, sheria za forodha zinapiga marufuku au kudhibiti uingizaji wa bidhaa fulani kama vile dawa zisizoidhinishwa, silaha, na bidhaa bandia. Ukiukwaji wa sheria hizi unaweza kusababisha faini kubwa, kutaifishwa kwa bidhaa, au hata kifungo jela.

Faida kubwa ya sheria hizi ni kulinda viwanda vya ndani kwa kudhibiti ushindani usio sawa kutoka nje. Pia husaidia kuongeza mapato ya serikali ambayo hutumika katika maendeleo ya miundombinu na huduma za kijamii kama afya na elimu.

Hata hivyo, changamoto bado zipo, ikiwemo uelewa mdogo wa sheria kwa wafanyabiashara wadogo, pamoja na urasimu unaoweza kuchelewesha shughuli za kibiashara. TRA imekuwa ikiendelea kuboresha mifumo ya kidigitali ili kurahisisha taratibu na kuongeza uwazi.

Kwa ujumla, uelewa wa sheria za kodi ya forodha ni muhimu kwa kila mfanyabiashara ili kuepuka hasara na kuhakikisha biashara inafanyika kwa kuzingatia sheria za nchi. Alpha Habari inaendelea kuhamasisha elimu ya kodi kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa Tanzania.



## KONA YA MASWALI KWA WASOMAJI

1. Ni mfumo upi wa kidijitali unaotumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kurahisisha taratibu za forodha, kupunguza ucheleweshaji, na kuongeza uwazi?
   A. IDRAS B. TANCIS
   C. EFD D. SimBanking

2. Majukwaa ya kimataifa ya kidijitali kama Netflix yanatakiwa kutoza kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya asilimia ngapi kwa watumiaji wa Tanzania?
   A. 10% B. 15%
   C. 18% D. 20%

3. Kwa mujibu wa "Kona ya Mwanza", walipa kodi wadogo mara nyingi hutumia mfumo upi rahisi wa kulipa kodi ili kupunguza ugumu wa mahesabu?
   A. Kodi ya Makadirio (Presumptive Tax)
   B. Kodi ya Mapato ya Kampuni (Corporate Tax)
   C. Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)
   D. Kodi ya Forodha

4. Sheria kuu inayotumika kusimamia taratibu za forodha na ukokotoaji wa kodi katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inaitwa:
   A. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332
   B. East African Community Customs Management Act (EACCMA)
   C. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438
   D. Sheria ya VAT, Kifungu cha 47

5. Chama cha Washauri wa Kodi Tanzania (TATC) kimependekeza kuwa salio la kodi iliyozidi (withholding tax au provisional tax) lifanyiwe nini? A. Lifutwe baada ya mwaka mmoja B. Lirudishwe kwa mlipakodi ndani ya siku 7 C. Liweze kuhamia miaka inayofuata hadi litumike kikamilifu D. Ligeuzwe kuwa faini ya kiutawala

5.

A. Lifutwe baada ya mwaka mmoja
B. Lirudishwe kwa mlipakodi ndani ya siku 7
C. Liweze kuhamia miaka inayofuata hadi litumike kikamilifu
D. Ligeuzwe kuwa faini ya kiutawala

6. Eleza faida nne (4) za kodi ya forodha katika kukuza uchumi wa Tanzania.

7. Fafanua utofauti wa usimamizi kati ya "Walipa Kodi Wakubwa" na "Walipa Kodi Wadogo" kama inavyoelezwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

8. Je, mfumo wa Kodi ya Huduma za Kidijitali (Digital Services Tax - DST) unafanyaje kazi kwa kampuni za nje kama Google na Meta ambazo hazina ofisi za moja kwa moja nchini Tanzania?

9. Eleza maana ya mfumo wa EFD (Electronic Fiscal Device) na umuhimu wake katika kudhibiti ukwepaji kodi nchini.

10. TATC inatumia mbinu gani kitaaluma kuwasilisha changamoto na mapendekezo ya wafanyabiashara kwa serikali badala ya kutumia malalamiko yasiyo na mwelekeo?

- Walengwa wa maswali haya na wanao takiwa kujibu ni wanafunzi wa vyuo vikuu na wafanyabiashara
- Majibu yote yatumwe kupitia barua pepe md@alphaassociates.co.tz au nambari ya whatsaap 0768449886.
- Watakao jibu vyema na kwa usahihi watapata zawadi
- Jibu Maswali yote 8 ili ujihakikishie ushindi
- Washindi watano watapewa zawadi na kutatangazwa katika toleo la Aprili
- Mwisho wa kutuma/kuwasilisha majibu ni tarehe 20/2/2026.

kwa msaada/ maelezo zaidi tupigie 0768449886.
Vigezo na masharti kuzingatiwa.

# MIAKA 25 YA ALPHA ASSOCOATES TANZANIA LTD NA HUDUMA ZA KIKODI NCHINI TANZANIA

Alpha Associates Tanzania Limited ilianzishwa mwaka **2000,** ikiwa na lengo la kutoa huduma za kitaalamu katika masuala ya **uhasibu, ushauri wa kikodi, na usimamizi wa biashara.**

Katika kipindi cha zaidi ya robo karne:

- Imehudumia mamia ya wateja (SMEs, taasisi, na watu binafsi)
- Imejijengea sifa ya kuwa mshauri wa kuaminika katika masuala ya kodi
- Imechangia kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na uwajibikaji wa kifedha kwa biashara nyingi

**Utekelezaji wa huduma za kikodi nchini Tanzania**

Kwa miaka 25, kampuni imekuwa mstari wa mbele katika kusaidia utekelezaji wa sheria na mifumo ya kodi kupitia:

1. **Uzingatiaji wa kodi (Tax Compliance)**
   - Kusaidia wafanyabiashara kufuata sheria za kodi kama VAT, PAYE, SDL, WHT na income tax
   - Kuandaa na kuwasilisha marejesho ya kodi kwa wakati

Kupunguza hatari ya adhabu na ukaguzi

**2. Ushauri wa kikodi (Tax Advisory)**

- Kutoa mikakati ya kupanga kodi (tax planning)
- Kusaidia kupunguza mzigo wa kodi kisheria
- Kushauri biashara katika mabadiliko ya sera za kodi

**3. Msaada wa ukaguzi (Audit & Investigation Support)**

- Kuwawakilisha wateja mbele ya Tanzania Revenue Authority (TRA)
- Kuandaa nyaraka muhimu wakati wa ukaguzi wa kodi

Kusaidia kutatua migogoro ya kikodi

**4. Mafunzo na uhamasishaji**

- Kutoa warsha na mafunzo ya kodi kwa wafanyabiashara na taasisi
- Kukuza uelewa wa sheria za kodi kwa jamii
- Kuchangia ukuaji wa uchumi rasmi (formalization ya biashara)

**5. Usajili na urasimishaji wa biashara**

- Kusaidia biashara kuingia kwenye mfumo rasmi
- Kuweka mifumo ya uhasibu na ripoti sahihi
- Kuongeza uwazi na uwajibikaji wa kifedha

Katika miaka 25, mchango wa Alpha Associates umeonekana katika Kuongeza uelewa wa kodi kwa wafanyabiashara, Kusaidia kuongeza mapato ya serikali kupitia ufuataji wa sheria, Kukuza nidhamu ya kifedha na uwazi katika sekta binafsi na Kuimarisha mazingira ya biashara Tanzania.

Hitimisho

Maadhimisho ya miaka 25 ya Alpha Associates Tanzania Limited si tu kumbukumbu ya safari ndefu ya kibiashara, bali pia ni ushahidi wa mchango wa kampuni katika kujenga mfumo imara wa kodi na biashara nchini Tanzania. Ni taasisi iliyochangia kwa kiasi kikubwa kuifanya kodi iwe rahisi kueleweka, kufuatwa, na kuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi.

